# *Ni Mimi, Msiogope*

Baba wa Mbinguni mwenye neema, tunashukuru... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...usiku wa leo kwa ajili ya Yesu, Mwanao, Ambaye alikuja duniani na kufanywa dhambi, akichukua mahali petu na kufa msalabani, ili sisi kwa njia ya haki Yake tupate kuhesabiwa haki kwa imani yetu katika kazi Yake, tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili, kwamba tuna majaliwa haya katika saa ambazo hakuna tumaini katika kitu kingine chochote.

2 Wakati matumaini yote ya usalama wa taifa, ama matumaini yote ya maisha ya nyumbani yamevunjika, taifa limevurugika, mataifa dhidi ya mataifa, falme dhidi ya falme, maumbile yenyewe yanapaza sauti, mwisho umekaribia, matetemeko ya nchi mahali mahali, mawimbi ya bahari, bahari inanguruma, tuna furaha sana kwamba kuna "Mwamba ulio juu kuliko mimi; Kimbilio wakati wa..." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili. Tungeomba, Baba, ya kwamba Yeye angeendelea kuwa pamoja nasi tunapoendelea na safari. Lifanye kuwa tukio maalum usiku wa leo, Baba.

3 Tumegawa kadi nyingi za maombi alasiri ya leo, ambapo watu hawa wataombewa, walio wagonjwa. Jalia kusiwe na mtu mnyonge miongoni mwetu ibada itakapokwisha. Jalia kila mwenye dhambi, wakati Ndugu yetu Daudi anapofanya wito wa madhabahuni, kama kawaida, usiku, tunaomba, Baba, kwamba wenye dhambi, kila mwanamume ama mwanamke aliye hapa ndani ambaye si Mkristo, jalia wakukubali Wewe kama Mwokozi wao binafsi, jalia waliorudi nyuma waje nyumbani kwa Mungu, wakitambua ya kwamba wakati umewadia. Tunaomba haya, katika Jina la Yesu. Amina.

4 Mwaweza kuketi. (Asanteni.) Hii imekuwa siku isiyo ya kawaida kwangu. Nimekuwa na majaliwa makuu leo ya kutembelea mashirika ya Abundant Life na *Faith Digest*. Loo, jinsi ninyi watu hapa mlivyo na bahati kuwa na kitu kama hicho mjini mwenu! Jinsi ambavyo Mungu amewachukua wavulana waliokuwa wakisimama pembeni hapa Sand Springs, wakiwa na kodiani, hao wawili pamoja, na kufanya mkutano wa mtaani, na leo hii karibu wameushika ulimwengu mikononi mwao, kwa Injili hii kuu. Jinsi ninavyomshukuru Mungu kutoka kwenye kilindi cha moyo wangu, kwamba Yeye aliwahi kuwatuma watu hao. Bwana na aendelee kumbariki Ndugu Oral Roberts na Ndugu Tommy Osborn.

5 Sasa, daima inauchangamsha moyo wangu kumwona Bwana akiwasaidia watu Wake, akifanya jambo ambalo—ambalo lina faida.

6 Kila usiku ninaona leso kadhaa zimewekwa hapa, na barua. Sasa, tunaamini jambo hilo, kuombea vitambaa hivyo. Sasa, nimekuwa nikisoma zingine zilizosema, "Waweza kupaka leso hii mafuta, Ndugu Branham?"

7 Vema, kupaka leso mafuta ni sawa kabisa, nasi tunaamini ya kwamba chochote ambacho Mungu atabariki, tuko tayari kukipokea, lakini ukiangalia katika Maandiko, hazikutiwa mafuta, "Walikuwa wamechukua kutoka kwenye mwili wa Paulo leso na nguo." Ninaamini Paulo alikuwa mtu wa kimsingi, sivyo? Kwa hiyo, nafikiri mahali alipotoa hilo palikuwa ni katika hadithi ya yule mtoto wa Mshunami aliyefufuliwa, ama, mvulana mdogo aliyefufuka katika wafu.

8 Kumbukeni, alimwambia Gehazi, "Chukua fimbo hii uende ukaiweke juu ya huyo mtoto mchanga." Alijua ya kwamba kila kitu alichogusa kilibarikiwa. Lakini imani ya huyo mwanamke Mshunami haikuwa katika hiyo fimbo, ilikuwa katika nabii, kwa hiyo alikaa pamoja naye mpaka alipoenda na kuulaza mwili wake mwenyewe juu ya huyo mtoto mchanga, ndipo akafufuka.

9 Sasa, tuna huduma kuu ya hii, si huduma kuu kama waliyo nayo hawa ndugu hapa, bila shaka.

10 Nilikuwa nikiona, nilipokuja nyumbani, nilimwangalia Billy, nikasema, "Unajua, ofisi yangu itaonekana ni duni sana tangu sasa na kuendelea." Nina taipureta mbili zilizowekwa mwishoni mwa trela, huo ndio ukubwa wa yangu. Lakini nikasema, "Itaonekana ndogo sana tangu sasa na kuendelea."

11 Lakini jinsi ambavyo humo ndani tunaombea leso, vipande vidogo vya nguo, na kuvituma kote ulimwenguni, kila mahali. Naye Bwana hubariki jitihada zetu dhaifu za kuwasaidia watu.

12 Na sasa, usipopata moja mkutanoni, nawe ungetaka moja, vema, nitafurahi kukutumia, niandikie tu. Nami nina-. . . Mimi, ninafanya vizuri kupata za kutosha kuwalipia wale wanaotufanyia kazi, wachache pale kwenye dawati, kwa hiyo huenda tukachelewa kidogo kulijibia, bali tutafanya kila tuwezalo kukutumia moja kwa moja bila malipo. Kwa hiyo, tuma ukitaka.

13 Sasa, Ndugu du Plessis ndiye mnenaji, naye kwa kawaida huzungumza kila usiku, basi nitakapoingia ingekuwa ni vema kuanzisha tu mstari wa maombi. Sasa, leo tumeamua, nilimwambia mwanangu aje huku na kugawa lundo la kadi za maombi, ili tuweze kuwaombea wagonjwa usiku wa leo kwa kuwapitisha kwenye mstari wa maombi na kuwaombea.

14 Kila usiku tumemtegemea Roho Mtakatifu ajitokeze, sasa, na kuwaita watu, na kuwajulisha Uwepo Wake upo hapa.

15 Sasa, siamini ya kwamba kuna mtu yeyote duniani anayeweza kukuponya, hiyo ni hata kwa daktari. Uponyaji ni

wa Mungu pekee, “Mimi ndimi Bwana nikuponyaye magonjwa yako yote.”

16 Sasa, tunamshukuru Mungu kwa ajili ya madaktari wetu na hospitali zetu, nasi kamwe hatujaribu kuwahukumu. Lakini hakuna dawa itakayouponya mwili wako, sasa, kumbuka tu hilo, hakuna dawa iliyowahi kuvumbuliwa, wala haitavumbuliwa kamwe, itakayoponya. Hebu mpe mmoja, itamsaidia, mpe huyo mwingine, nayo itamwua, kwa hiyo hakuna uponyaji.

17 Kwa mfano, kama nikiukata mkono wangu, hakuna dawa ulimwenguni ya kuuponya mkono wangu, jeraha la kawaida la kisu. Kama ingeponya jeraha la kisu mkononi mwangu, ingeponya mkato wa kisu kwenye koti langu, ingeponya mkato wa kisu kwenye dawati hili.

18 Ndipo huenda ukasema. . .[Ndugu Branham anakohoa—Mh.] (Samahani.) Huenda ukasema, “Ndugu Branham, dawa haikutengenezwa ikaponye koti lako, ilifanywa ili kuuponya mwili wako.” Vema.

19 Kama nikiukata mkono wangu, nianguke nife, nao wangenipeleka kwenye kituo cha mazishi na kuutia mwili wangu dawa ya kufanya usioze ambayo ingenifanya nionekane wa kawaida kwa miaka hamsini. Kila siku madaktari bora zaidi ulimwenguni wangeweza kuja, waushone huo, wanidunge sindano ya penisilini, waupake marhamu, na kadhalika, juu yake, na miaka hamsini tangu sasa hilo jeraha lingeonekana kama tu lilivyokuwa wakati nilipoukata.

20 “Mbona,” unasema, “hakika, uhai umekutoka.”

21 Basi ni gani mponyaji, dawa au uhai? Uhai ndio mponyaji. Mnaona, dawa haiwezi kujenga tishu.

22 Kama nilikuwa nikizungusha mpini wa gari langu nikauvunja mkono wangu, jambo la kwanza, ningeenda, niseme, “Daktari,” niingie, niseme, “rudisha mkono wangu.” Vipi kama ningeingia, niseme, “Uponye mkono wangu, Daktari, ninataka kumaliza kuzungusha mpini wa gari langu”?

Angesema, “Mbona, unahitaji uponyaji wa akili, jamani.” Naye angekuwa sahihi, kwa sababu asingeweza kuuponya mkono wangu.

“Vema,” ningesema, “kwani wewe si mponyaji?”

23 Angesema, “La, hasha.” Angesema, “Nitarudisha mkono wako, niuweke mahali pake, lakini Mungu hana budi kuuponya.” Hiyo ni kweli. Mungu ndiye Mponyaji pekee aliyepo.

24 Nimehojiwa kwenye Mayo Brothers na kliniki nyingi mashuhuri, na kamwe bado sijawahi kuona moja ya kuniambia walikuwa waponyaji. Wao. . .Katika Mayo ya kale, ambako walinipeleka, na kunionyesha ile ishara kubwa aliyokuwa nayo, ilisema, “Hatudai kuwa waponyaji, tunakiri tu kusaidia

maumbile, kuna Mponyaji mmoja, huyo ni Mungu." Hiyo ni kweli.

25 Nilitoa tamshi hilo wakati mmoja, ndipo mtu fulani baada ya ibada akanishika na kusema, "Vipi kuhusu penisilini, Ndugu Branham? Inaua vijidudu vya mafua."

26 "Vema," nikasema, "penisilini ni kama tu ulikuwa na nyumba iliyojaa panya wakitoboa mashimo kila mahali, nawe ukamwaga sumu kidogo ya panya na kuwapa hao panya sumu, hiyo haizibi hilo shimo, hiyo inawaua tu panya." Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo penisilini ama dawa nyingine yoyote hufanya, inaninii tu, wakati mwingine viuavijasumu, na kadhalika, huua kijidudu, bali Mungu hana budi kuuponya. Hiyo ni kweli. Uponyaji wote ni wa Mungu. Kwa hiyo wewe uwe mwema tu kwa Mungu, mwamini Mungu, Mungu atayashughulikia hayo mengine. Hiyo ni kweli.

27 Kwa hiyo tunawaombea wagonjwa, hatuwaponyi wagonjwa. Nimeona makumi ya maelfu ya wagonjwa wakiponywa, kuponywa kabisa, wanne wenye kumbukumbu za kufufuka kutoka kwa wafu katika huduma yangu ndogo, ila sijawahi kumponya mtu yeyote bado. Ni imani yao katika kazi iliyomalizika ambayo Kristo alifanya pale Kalvari, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa."

28 Na sasa, imani yako katika kazi hiyo iliyomalizika ndiyo inayofanya kazi. Hivyo ndivyo ilivyo. Unakiri, Naye ni Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, hawezi kukufanyia lolote, mpaka kwanza ukiri kwamba wewe…isipokuwa ukiri yale Yeye aliyosema, "Kwa kupigwa Kwake mimi niliponywa." Basi Yeye ni Kuhani Mkuu kutuombea tunapokiri. Na kama hiyo siyo Injili, siijui, nami nimeninii, nimekuwa makosani, bali nimemwona akifanya hivyo kupita kiasi.

29 Mtu fulani, m—mhudumu fulani aliniambia wakati fulani uliopita, kasema, "Sijali kama ninii…kama kivuli cha mtu mwenye kansa kingeinuka vizuri kabisa, sijali ungesema nini, siamini."

30 Nikasema, "La, hasha, haikuwa kwa ajili ya wasioamini, ilikuwa tu ni kwa ajili ya waaminio, ilikusudiwa hao tu." Wasioamini hawataliona kamwe, mnaona, halikukusudiwa wasioamini, lilikusudiwa waaminio. "Yeye aaminiye, yote yanawezekana."

31 Kwa hiyo, tuna…Marekani imejaa waaminio wa Kiyahudi, Wayahudi walikuwa na desturi ya kuwekea mikono. Hilo kamwe halikuwa kwa Kanisa la Mataifa, la, bwana, lilikuwa ni kwa ajili ya Wayahudi pekee.

32 Kama ukiangalia, kulikuwa na kuhani aliyemwambia, Yairo—Yairo alimwambia Yesu, "Njoo, umwekee mikono binti yangu, naye ataishi," alikuwa mahututi, "uweke mikono Yako juu yake."

33 Lakini kwa yule Mrumi, Mmataifa, alisema, "Sistahili Wewe uje chini ya paa langu, sema tu Neno, mtumishi wangu ataishi." Mnaona tofauti yake?

34 Huko Afrika, tulifanyiza mstari wa maombi, na yapata watu watatu au wanne walikuwa wamepitia kwenye mstari wa maombi huko Durban, Afrika Kusini, anakotoka Ndugu du Plessis, nao walikadiria waongofu elfu thelathini katika dakika chache baada ya hapo. Watu elfu thelathini walimpokea Yesu Kristo kama Mwokozi binafsi.

35 Na maelfu, Ndugu Bosworth alikadiria, maskini Daddy Bosworth, loo, karibu ninyi nyote mlimjua, ninasahau ni elfu ngapi alizokadiria za walemavu, na viwete, na vipofu, vilema, walioacha fimbo zao, na mikongojo, na vitanda vimetandazwa papo hapo chini, nao wakaondoka kwa sababu waliliamini. Walikuwa wameona kitu halisi, nao wakaamini.

36 Lakini kwa namna fulani, na hapa nyumbani tunataka watu wawekewe mikono, hao ni "Na iwe kwenu kulingana na imani yenu." Kwa hiyo, daima tuna furaha kuwaombea wagonjwa. Lakini njia halisi kwetu kuipokea ni kujua ya kwamba imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno.

37 Sasa, kama mnaweka kumbukumbu ya mazungumzo haya madogo kwa yapata dakika kumi na tano tu, ningependa kufanya mchezo mdogo tu wa kuigiza usiku wa leo kidogo nipate kuuhisi mkutano. Nami ninataka kusoma kutoka katika Injili ya Mathayo Mtakatifu mlango wa 14, na kifungu cha 27:

> *Mara Yesu akasema nao, akawaambia, Jipeni moyo; ni mimi; msiogope.*

38 Jinsi ninavyoyapenda Maandiko hayo!

39 Hapana shaka ilikuwa karibu machweo, kadiri niwezavyo kuwazia, wakati yule mvuvi mkubwa mwenye misuli migumu mgongoni alipousukuma ule mtumbwi mdogo ziwani, akapanda mwenyewe, kisha akapanda moja kwa moja kupitia vitini, akapata mahali pake karibu na ndugu yake Andrea, akaketi chini, huku kila mmoja akichukua makasia na kuanza kuvuta maskini mashua kwenye ziwa laini, ikaelea upesi kuingia ziwani.

40 Baada ya yule wa mwisho kupunga mkono wa kwaheri kutoka ufukoni, akiwapungia mkono wa kwaheri walipokuwa wakivuka ziwa, nao wakafika umbali wa kutosha ambapo wasingeweza kuona wala kupunga mkono tena, hapana shaka ilikuwa ni kijana Yohana aliyesimama kwa dakika moja, na kuinua mkono wake kupangusa jasho kutoka kwenye paji la uso wake, kasema, "Ndugu, nilipokuwa mvulana mdogo tu, ninaweza kukumbuka jinsi mama alivyokuwa akinichukua mikononi mwake na kunisomea Maandiko Matakatifu, jinsi alivyozoea kusoma na kuniambia kwamba wakati watu wetu walipokuja kwenye nchi hii nzuri, wakija kutoka Misri ambako walikuwa utumwani kwa miaka mia nne, kwamba Yehova

Mungu mkuu alinyesha mikate kutoka Mbinguni na kuwalisha watu wetu kwa muda wa miaka arobaini nyikani.

41 "Nami ninaweza kukumbuka jinsi nilivyokuwa nikisema, 'Mama, hivi Malaika walioka mikate hiyo na kuwapelekea watu wetu?'

42 "Naye angeniambia, 'Mtoto Johnny, siamini ya kwamba Malaika walioka mikate hiyo, ninaamini ya kwamba Mungu Muumba mkuu wa Mbingu na nchi alinena tu Neno na akaumba mikate hiyo iliyowalisha watu wetu.'

43 "Na sasa, ndugu, mlionaje alasiri ya leo mlipomwona Yeye akichukua hizo biskuti ndogo tano na samaki wawili na kuwalisha elfu tano? Hakika, hatumfuati mtu bandia kama watu wanavyosema tunamfuata. Mtu huyo ana uhusiano fulani na Yehova Mungu, kwa sababu Yeye angeweza kuumba mkate moja kwa moja mikononi Mwake. Siamini," huenda alisema, "kwamba Mtu huyo ni nabii wa uongo, ninaamini ya kwamba tunamfuata Mwana wa Yehova Mungu."

44 "Vema," akasema Simoni, yule mvuvi mkubwa, "kweli, moja kwa moja tu kule ambako mimi na Baba tulikuwa tukivua samaki miaka mingi iliyopita, aliniambia siku moja, 'Ninazeeka, Simoni, nami nimejaribu kumtumikia Mungu maishani mwangu mwote, na nimeishi kwa uaminifu tu nijuavyo, nami nimekulea, mvulana wangu, kumwamini Mungu yeye yule. Lakini inaonekana kana kwamba labda sitamwona Yule aliyeahidiwa, lakini wewe ni mvulana mdogo, bado, huenda ukamwona. Na sasa, mwanangu, kabla sijaondoka, nataka kushindilia hili moyoni mwako.'"

45 Huenda Petro alisema hivyo, ya kwamba baba yake alikuwa akizungumza, akisema, "'Mwanangu, kamwe usiyaondokee Maandiko kwa jambo lolote linakalotukia, dumu na Neno.

46 "'Sasa, nabii Musa alitwambia ya kwamba Bwana Mungu wetu atatuondokeshea Nabii miongoni mwetu siku moja miongoni mwa watu wetu, na Mtu huyu angekuwa ndiye Masihi. Yeye anapaswa kuwa Mwanadamu, Mtu wa kawaida tu aliyeinuliwa miongoni mwetu. Lakini jinsi utakavyomjua, mwanangu, Yeye atakuwa ni Nabii, nawe utakumbuka ya kwamba Huyo ndiye Masihi ajaye. Siku nyingi zimepita tangu nchi hii iwe na nabii.'

47 "Na ndipo Andrea alipokuja siku hiyo na kunisimulia baadhi ya hadithi hizo kuhusu huyu Yesu wa—wa Nazareti, nililitilia shaka, ndugu, moyoni mwangu, kweli nililitilia shaka. Ndipo nikasema, 'Andrea, unaota ndoto za mchana, rudia fahamu zako.' Nami nikamsumbua vibaya sana.

48 "Lakini siku moja alinishawishi niende, ndipo nilipokuja karibu na huyo Mtu, niliona hapakuwapo na jambo lisilo la kawaida kwake, bali Yeye aligeuka, akaniangalia, na kusema, 'Jina lako ni Simoni, na baba yako alikuwa ni Yona.'

49 "Si kwamba tu alinijua mimi bali alimjua maskini yule babangu mzee mtauwa. Hilo lilitosha kwangu, ndugu. Niliamini papo hapo, kabla sijamwona akiumega mkate wowote na kuubariki, niliamini ya kwamba huyo alikuwa ndiye Masihi, kwa kuwa baba yangu alikuwa amenisomea kutoka katika Maandiko, nami najua Maandiko hayasemi uongo. Kwa hiyo, niliridhika kwamba huyo alikuwa ndiye Masihi."

50 Hapana shaka ilikuwa ni yapata wakati huo ambapo—ambapo huenda Filipo alisema, "Lakini, ndugu, laiti mngaliuona uso wa Nathanaeli, Ndugu Nathanaeli aliyeketi pale kichwani mwa chombo, laiti mngaliona uso wake siku hiyo alipokuwa, tulikuwa tukijadiliana, na nilipomleta Mbele za Yesu, nami nilikuwa nimemwambia mambo yaliyokuwa yakitukia, lakini akasema, 'Loo, hilo ni—hilo ni jambo tu unalowazia.'

51 "Lakini wakati alipokuja Mbele za Yesu, Yeye alimwambia kile alichokuwa, kwamba alikuwa mtu mwaminifu, mtu mwema, nalo likamshangaza Ndugu Nathanaeli, lakini alipomwambia mahali alipokuwa kabla hajaja mkutanoni, Nathanaeli alishawishika ya kwamba huyo alikuwa ndiye Mwana wa Mungu."

52 Ndipo Andrea mkubwa, akimkumbatia Simoni, huenda alisema kitu kama hiki: "Lakini sisi sote tulijisikiaje wakati Yeye alipotutuma mjini kununua mikate? Kisha tuliporudi, tulimsikia akizungumza na mtu fulani, nasi tukasogea karibu kusikiliza ilikuwa ni kitu gani. Na huyo hapo alikuwa mwa—mwanamke mwenye sifa mbaya amesimama, akizungumza Naye kwenye lango la Samaria, kisimani.

53 "Nasi tukamsikia akimwomba aende akamwite mumewe. Nasi tukaangaliana. Naye akasema, 'Sina mume.' Tukawazia papo hapo ameteleza, mahali fulani. 'Sina mume.'

54 "Basi, ila Yeye akamtazama moja kwa moja usoni, na kusema, 'Umesema vema. Kwa maana umekuwa na waume watano; na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.'

55 "Ndugu, mliona sura ya mwanamke huyo? Upesi, akageuka, na kusema, 'Bwana, hapana shaka Wewe ni nabii. Tunajua Masihi atakuja, Naye atatuambia mambo haya.'

56 "Na ndipo akampa mwanamke huyo faraja hiyo itoshelezayo kwa yote, iridhishayo, na kusema, 'Mimi ninayesema nawe Ndiye.'

57 "Mliona sura yake? Alipogeuka akiwa na mtazamo huo wa amani usoni mwake, akikimbia mjini, akipiga mayowe kutoka pande zote mbili, 'Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Je, haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi tunayemtazamia? Si Huyu ndiye yule Nabii ambaye Musa alisema atainuka katika siku za mwisho, atakuwa

Mmoja miongoni mwetu? Yuko huko nje kisimani sasa, Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya.'

58 "Nanyi mliona, ndugu, wakati hao Wasamaria walipokuja kutoka mjini, hawakumwomba Yeye arudie hayo hata wakati mmoja? Waliridhika kwamba Huyo alikuwa ndiye Mtu huyo, nao walilijua."

59 Maskini huo mtumbwi mdogo ulipokuwa ukienda mbio kuvuka hilo ziwa, hapana shaka ilikuwa yapata wakati huo ambapo hapana shaka Shetani aliinuka, na kusema, "Loo, nimewashika peke yao bila yeye! Sasa ni wakati wangu wa kumalizana nao, kwa kuwa walikuwa wakiwatoa pepo wangu, na kadhalika, kwa hiyo nitawajutisha."

60 Hapo ndipo Shetani anapoweza kujilipizia kisasi, anapoona kwamba umeondoka bila Yesu. Hapo ndipo Shetani atakapolipata kanisa, wakati mnapovutiwa sana na jambo lingine mbali na mikutano ya maombi, mnapovutiwa sana kwamba—kwamba mnapaswa kupata mafanikio ya kawaida badala ya mafanikio ya kiroho, basi kumbukeni, Shetani yuko njiani mwake, amewashika bila Yeye.

61 "Ee Mungu," ndilo ombi langu, "liamshe kanisa, tena, kwenye mikutano ya maombi ya mtindo wa kale, ya usiku kucha. Waamshe watu kwenye mazingira ya—ya kiroho." Loo, i—inahitaji hayo kuwaleta watoto katika Ufalme, inahitaji hayo mazingira.

62 Moja kwa moja usiku huu, wakati tumeketi hapa, kama mazingira haya mazuri yangetukia, kundi hili lote lingejazwa tena na Roho Mtakatifu, kila mgonjwa angeponywa, mazingira ndiyo yanayofanya jambo hilo.

63 Unaweza kuchukua yai la kuku na kuliweka kwenye kiatamia na kuweka mazingira sawa, kitaangua kuku, si kiangulio. Mnaona? Kwa sababu hayo ndiyo mazingira yanayojalisha. Hebu weka yai la kuku chini ya m—mbwa, atamwangua kuku, ni mazingira.

64 Na hilo ndilo linalohitajika kanisani siku hizi, si sana sana kanuni baridi za imani na theolojia, bali Roho wa Mungu aliye hai akishuka juu ya watu Wake kuleta mazingira ya kiroho, si mmoja akisema, "Ninaamini ni *hiki*," mwingine, "Ninaamini ni *kile*." Ni vigumu kwa Roho Mtakatifu kufanya kazi.

65 Unajua ni lini Roho Mtakatifu alipokuja mara ya kwanza? Ilikuwa kwenye Siku ya Pentekoste, wakati wote walikuwa mahali pamoja na nia moja. "Na ndipo kukaja kutoka Mbinguni uvumi kama upepo wa nguvu ukienda kasi." Iliwabidi kuweka mazingira sawa. Hilo ndilo tunalohitaji siku hizi, ndugu. Tuko nyuma kabisa, kanisa linapaswa kuwa limeenda maili milioni moja safarini.

66 Tunapochukua kama yale yaliyotukia kule Afrika hivi majuzi wakati Ndugu yetu wa thamani Billy Graham, wakati huyo Mhindu alipopanda huko nje na kutoa changamoto namna hiyo dhidi ya Neno la Mungu aliye hai, inaonyesha tunahitaji mazingira mengine badala ya theolojia, tunahitaji nguvu za Roho Mtakatifu miongoni mwetu, watu walio tayari kusimama juu ya yale Mungu aliyosema kuwa ni kweli. Ni mazingira tunayohitaji.

67 Labda, katika siku hii kuu ya mafanikio, ambapo tumevutiwa sana na mafanikio hata tumeacha jambo lililo muhimu. Labda tumeenda kombo kwa namna fulani ya hamaki bila Yeye, haitupasi kufanya hivyo, ni mazingira, ni mahali ambapo tu—tunamtaka Kristo.

68 Sasa, Yeye hakwenda mbali sana nao wakati alipojua ya kwamba wangemhitaji. Ninaamini ya kwamba Yeye anajua usiku wa leo kwamba tunamhitaji, tunajua leo kwamba tunamhitaji. Ninamhitaji, unamhitaji, sote tunamhitaji. Ninamhitaji zaidi, unamhitaji zaidi. Kuna jambo moja ambalo siwezi kuridhika nalo, kutosheka na Mungu.

69 Loo, na kadiri tuwezavyo kujiachilia, basi Mungu anaweza kuingia, bali inatubidi kujiondoa njiani, mawazo yetu wenyewe, kumwacha Roho Mtakatifu aingie na kutuonyesha mambo yajayo, alisema angefanya hivyo, na kutukumbusha mambo.

70 Sasa, Yesu, akijua ya kwamba hao wanafunzi watapata matatizo, alipanda kilima kirefu kuliko vyote angaliweza kupanda, huko juu kabisa mlimani kusudi aweze kuona kote ziwani, kwa kuwa Yeye alijua mahali fulani mle ndani ya kwamba wangepata matatizo. Mara walipoondoka asiweze kuwaona, ama, kutoka Uweponi Mwake, Yeye alijua ya kwamba Shetani angewafuatilia.

71 Basi akapanda mlima mrefu zaidi ili aweze kuangalia kote kote baharini, na kuwaangalia mpaka walipofika mwisho wa safari. Hakuwafanyia hivyo tu, bali alipanda mlima mrefu kuliko yote ungeweza kupandwa, alipanda Mlima Kalvari, na kutoka hapo akaenda juu zaidi ya mwezi na nyota, kote kote hata Mbinguni, kusudi aweze kuona kutoka Umilele hata Umilele, kwa kuwa alijua Kanisa Lake lingekuwa katika uhitaji.

72 Naye, "Jicho Lake liko kwenye shorewanda," nami ninajua Yeye anauangalia mkutano huu usiku wa leo, akijaribu kumpata mtu aliye na imani ambaye atamwamini, wala asitilie shaka, na kusukuma kila mahali, na kufanya kila namna ya vitu bandia, bali ataamini urahisi wa Mungu katika Neno Lake ndilo alilosema kuwa ni kweli.

73 Alipanda kwenye ngome za Utukufuni, akapanda juu ya mwezi na nyota katika kufufuka Kwake. Nabii alisema alipofika juu sana kule, kwamba labda Yeye na watakatifu wa Agano la Kale wakipanda juu. . . Mbona, ninaweza kuwaona Malaika

wakiangalia juu ya lango, nao wakapiga mayowe mle ndani, watakatifu wa Agano la Kale walisema, "Inukeni, enyi malango ya milele, mkainuke, Mfalme wa Utukufu apate kuingia."

Nao Malaika waliokuwa nje ya malango wakasema, "Ni nani huyu Mfalme wa Utukufu anayeingia?"

"Bwana wa majeshi, shujaa wa vita."

74 Basi wakabonyeza kitufe, yale malango makubwa yakafunguka, ndipo Yesu na watakatifu wa Agano la Kale wakashuka kwenye barabara hiyo, washindi, loo, jamani, mpaka kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, na kusema, "Hawa hapa, Baba."

75 "Simama mkono Wangu wa kuume, hata nitakapowaweka adui wote chini ya miguu Yako." Na leo hii Yeye ameketi pale katika nguvu na utukufu akifanya ulinzi, kama tu yule tai wa kale.

76 Nilikuwa nimepanda juu ya majabali siku moja, nikiwatafuta ng'ombe, ndipo nikaona dhoruba ikija, naye maskini mama tai alikuwa amewapeleka makinda wake bondeni. Nao walikuwa kule chini wakiwa tu na yubile ya Kipentekoste, wakipinduana, mara ya kwanza waliyopata kutoka kwenye maskini kiota cha miiba, nao walikuwa kule chini wakicheza kama watoto wadogo.

77 Maskini huyo mama tai akaruka huko nyuma kabisa hadi kwenye jiwe kubwa, refu, kisha akakunja mbawa hizo kubwa, baadhi yao yana upana wa futi kumi na nne, naye akawaangalia hao watoto wachanga kupitia pale. Afadhali mbwa mwitu asimwendee mmoja, alikuwa anamwangalia. Alikuwa amesimama pale juu, na hayo macho makubwa, makali yangeweza kuona maili na maili.

78 Jicho kali kuliko yote yaliyopo, ni tai. Akiangalia chini... Mbona, anaweza, yeye...Kama mwewe angejaribu kumfuata, angesambaratika hewani. Kwa hiyo tai ni ndege aliyeumbwa maalum, naye hana budi kuwa na jicho maalum kusudi aweze kuona mahali alipo.

79 Mungu ni Yehova-Tai, Naye ameketi kwenye kiti cha Utukufu akiwaangalia watoto Wake, huru tu, akiwa na wakati mzuri.

80 Basi baada ya kitambo kidogo dhoruba ikatokea, maskini huyo mama tai akatoka kwenye mwamba huo, akaruka chini kupitia pale, na kupiga yowe. Tai hao wote wadogo wakashika mbawa zake kwa miguu yao, wakauma unyoya mzuri, mgumu kwa mdomo wao. Akaruka kwa hayo mabawa makubwa, akaingia kasi kwenye dhoruba hiyo, akaenda moja kwa moja kwenye shimo kwenye mwamba.

81 Nikamfunga farasi wangu na kuuzunguka-zunguka mti, nikipaza sauti kwa nguvu nilivyoweza, nikasema, "Loo, jicho Lake liko juu ya shorewanda, nami ninajua Yeye ananiangalia!"

82 Siku moja Yeye atatandaza mbawa Zake kubwa na kushuka chini. Ninataka kushika msalaba huo wa kale, unaoparuza na kuushikilia huo mpaka Roho Mtakatifu atakaponivuta kutoka kwenye machafuko haya tuliyomo siku hizi. Kama wewe ni mgonjwa usiku wa leo, shikilia ahadi ya Mungu ya msalaba wa ufufuo, shikilia hapo mpaka atakapokutoa nje.

83 Huyo hapo, matumaini yote yalikuwa yamekwisha . . . Labda uko usiku wa leo, labda daktari anasema huwezi kuishi tena. Labda unafikiri umevuka mstari wa utengano, huwezi kuokolewa. Hilo ni kosa, mradi tu una Mungu wa kutosha kuja hapa kwenye kanisa hili usiku wa leo, kuna matumaini kwako kuokolewa, mradi tu Roho wa Mungu anakushughulikia.

84 Na mradi tu una imani ya kutosha kuja hapa kuombewa, kuja chini ya mazingira ya Mungu aliye hai, chini ya ulinzi Wake na mbawa Zake, kama utaitumia tu imani hiyo, na kushikilia ahadi ya Mungu, utapona. Mungu aliliahidi, ni yale Mungu aliyosema.

85 Hapo, na ninii . . . Nadhani dhoruba inamulika, na radi kote angani, na yale mawimbi makubwa wakati ibilisi alipokuwa akipuliza sumu yake kutoka kinywani mwake namna hiyo, na kuleta mawimbi kotekote kutoka chini ya ziwa, pepo elfu kumi wameketi wakishangilia kote, "Tutawapata katika dakika chache! Kitambo kidogo tu, tutawapata!"

86 Kwa hiyo alipopulizia pumzi yake ya sumu kuyavuruga makanisa mengi, makusanyiko mengi makubwa, watu wengi, wazuri wa Kimarekani, akijaribu kuwapulizia sumu yake, na kusema, "Siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu," hayo tu ndiyo ajuayo, hayo tu ndiyo wajuayo. Ninawaambia, Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye ni yule yule.

87 Wakati yale mawimbi makubwa yalipokuwa yakienda, karibu sana matumaini yote ya kwamba wangepata kuokolewa, ilitokea walitazama, nao wakamwona akija akitembea kwa miguu juu ya maji. Lakini sehemu yake ya kuhuzunisha ilikuwa, enyi marafiki, waliogopa, walidhani ilikuwa ni mizuka.

88 Na hilo ndilo jambo lile lile ambalo limelipata kanisa siku hizi, wanaogopa tumaini pekee linaloweza kuwaokoa, tumaini pekee linaloweza kuwasaidia, wanaogopa. Nami ninaamini kama Yesu angeweza kuja kwenye mkutano huu usiku wa leo na kuonekana katika umbo la kimwili, katika mwili, Angesema mambo yale yale aliyosema pale: "Msiogope; ni mimi; changamkeni."

89 Ninaamini ya kwamba Yeye yupo hapa sasa, ninaamini ya kwamba Roho Wake Mtakatifu yupo hapa, kwa sababu

Yeye hufanya mambo yale yale anayofanya, huzaa aina ile ile ya tunda ambalo Yeye alizaa. Usiwe na shaka, tena, unawazuia tu waaminio wengine. Ingieni kwa nia moja, mseme, "Mungu, tunakushukuru kwa kututumia Roho Mtakatifu, nasi tunamwamini, na ni Wewe, nasi tunakukubali. Hatufikirii ni umizimu ama mizuka fulani, tunaamini ni Wewe, Bwana, kwa sababu Maandiko yalisema hivyo, Nawe uliahidi Hilo, nasi tuko hapa kumpokea."

90 Basi tunapowaombea usiku wa leo, wakati sio tu mimi ninayewaombea, bali kundi hili la wahudumu hapa, hawa hapa, kote hapa. Sisi si tu mmoja anaomba, sote tunaomba.

91 Kama ningekuwa mgonjwa huko nje, nikija kwenye mstari huu, ningewataka mniombee, kila mmoja wenu. Nami bila shaka, kama ningalikuwa na mtoto wangu mchanga huko nje, kama mke wangu angalikuwa akija kwenye mstari huo wa maombi, ningetaka kila mmoja wenu awe mwaminifu kabisa kulihusu. Na kama ungekuwa umesimama hapa kumwombea baba yangu, au mama yangu, ama dada yangu, ama ndugu, ama wapendwa, ningetaka uwe mwaminifu, ndugu. Nami nataka kuwa mwaminifu, pia.

92 Nami siwaambii chochote ila yale yaliyo Maandiko, Kristo tayari amemponya kila mmoja wenu. Mmeponywa kwa miaka elfu moja mia tisa, kwa kuwa alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa. Na kama angekuwa amesimama hapa usiku wa leo katika mwili wa nyama . . .

93 Mwili huo umeketi mkono wa kuume wa Mungu Mwenyezi. Utakaporudi, wakati hautakuwako tena, kutakuwako na Kunyakuliwa, nalo Kanisa litapanda kwenda kumlaki na kuwa pamoja Naye. Tutamlaki Bwana hewani atakaporudi. "Kuja Kwake kutakuwa kama radi iangazavyo toka mashariki, hata magharibi; ndivyo Kuja Kwake kutakavyokuwa." Na kila jicho litamwona, kila goti litapigwa, na kila ulimi utamkiri. Lakini Roho Wake Mtakatifu yupo hapa.

94 Tangu siku za Luther waliishi chini ya kuhesabiwa haki; siku za Wesley zikapanda juu kidogo, kanisa likawa katika uchache chini ya utakaso; ndipo ukaja uamsho wa Kipentekoste, ambao ulikuwa ni ubatizo wa Roho Mtakatifu, ama kurudishwa kwa karama; sasa tunaenda tu juu ya hilo, kwenye lile Jiwe la kifuniko. Kanisa halina budi kuwa kama . . . Roho aliye Kanisani na Roho aliye ndani Yake hana budi kuwa ni yeye yule.

95 Wakati Mungu alipothibitisha lile agano pamoja na Ibrahimu, hivi mliona yale aliyofanya, aliwachinja hao wanyama na kuwaweka hao hua, na kadhalika, mle ndani kisha akafanya agano? Agano ni nini?

96 Marekani tunasema, "Hebu na tufanye agano." Vema, tutakula chakula kidogo cha mchana, tutapeana mikono, na kusema, "Tutakubaliana." Hilo ni agano.

97 Huko Japani, unapofanya agano, wanarushiana chumvi. Hilo ni agano.

98 Huko mashariki, katika wakati wa Ibrahimu walipofanya agano, walimchinja mnyama, kama Ibrahimu alivyofanya, akagawanya ko—kondoo dume, na kadhalika, na mbuzi jike, chochote alichogawanya pale, wanyama watatu, na kuwatenganisha. Halafu basi, wakaandikiana agano lao kwenye kipande cha karatasi, wakasimama katikati ya hivi viwili, na kuwekeana nadhiri, kama wakivunja agano hili, miili yao na iwe kama yule mnyama aliyekufa.

99 Nao wakalipasua hilo agano, namna *hii*, mmoja akachukua kipande kimoja cha karatasi, mwingine hicho kingine. Ili kuthibitisha agano hili vipande vyote viwili ilibidi vije na kushikamana pamoja. Usingeweza kukinakili hata kama ingekubidi kufanya hivyo, hakungekuwa na njia ya kufanya hivyo, ilibidi uwe kitu kile kile.

100 Hivyo ndivyo Mungu alivyofanya pale Kalvari, Mungu alikuwa akimwonyesha Ibrahimu ya kwamba kupitia mwanawe Isaka angekuja Yesu, ndipo Mungu akampeleka Yesu Kalvari, na hapo akamrarua vipandevipande. Naye akauinua huo mwili na kuuweka kwenye mkono Wake wa kuume, kisha akashusha juu ya Kanisa Roho yule yule aliyekuwa juu Yake. Basi kwenye ufufuo, Roho aliyekuwa ndani ya Kristo itabidi awe ndani ya Kanisa, la sivyo hilo si agano.

101 Natumaini unaliona ndugu, dada. Roho aliyekuwa ndani Yake hana budi kuwa ndani yako, hilo ndilo agano Lake, Roho yule yule. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo, yeye naye atazifanya." Yuko hapa usiku wa leo.

102 Na tuinamishe vichwa vyetu. Je, kunaweza kuwako katikati yetu usiku wa leo mwanamume, mwanamke, ama mvulana, msichana, asiyemjua Yeye katika kusamehewa dhambi zao? Kama wangetaka kukumbukwa katika maombi haya kwamba, "Mungu unirehemu na unifanye chombo ambacho Wewe ungeweza kufanyia kazi." Kabla hujamwona Roho Mtakatifu akifanya jambo moja, waweza tu kuinua mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham, ninataka kumkubali Kristo"?

103 Mungu akubariki, bwana. Hiyo ni ninii halisi. . .Juu kwenye roshani, kwenye mkono wangu wa kulia. Hii. . .Mungu akubariki. Hilo ni sawa. Kadhaa. . .Katika roshani upande wa mbele, vema. Roshani upande wa kushoto, inua mkono wako sasa kama wewe si Mkristo. Nitawaomba tu. . .Mungu awabariki. Mungu awabariki, enyi wavulana. Chini hapa chini ya upande wa kushoto kwenye roshani, Mungu akubariki, ninauona mkono wako. Bila shaka, Mungu anakuona, hakika. Anajua yote kukuhusu. Vema.

104 Baba wa Mbinguni, waliinua mikono yao, ninaamini ni waaminifu, Bwana. Tunatambua ya kwamba hakuna muda

mwingi uliosalia, Yesu yuaja. Nasi tunaona ishara ya mwisho aliyolipa Kanisa ni pale alipojitangaza Mwenyewe kuwa ndiye Masihi.

105 Huyu hapa leo akiwa na Roho yule yule Kanisani Mwake, miongoni mwa watu Wake, akiwaponya wagonjwa, akitabiri mambo yatakayotukia, akiwaambia mambo ambayo yamekuwako, akiijulisha siri ya moyo, Yesu alijua mawazo yao. Na sasa, Baba, tunaona ya kwamba kitu hicho hicho kimekuja tena Kanisani, hakika Kuja Kwako kumekaribia.

106 Wasaidie watu hawa walioinua mikono yao, wapate kukupokea Wewe usiku wa leo kama Mwokozi wao binafsi, na kuokolewa kutoka kwa dhambi, na kujazwa na Roho Mtakatifu, wapate kuishi maisha ya Wakristo halisi waaminifu. Tujalie, Baba. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

107 Asanteni kwa dakika hizo ishirini. Na sasa, wewe uliyeinua mkono wako, wakati wito wa madhabahuni unapotolewa usiku wa leo na Ndugu yetu du Plessis, ninawatakeni mje hapa. Kama ulimaanisha hilo ulipoinua mkono wako, na kweli ulimaanisha hilo kutoka moyoni mwako, unajua Mungu aliamini neno lako papo hapo? Unajua ulivunja kila kanuni ya kisayansi ingeweza kuvunjwa ulipoinua mkono wako?

108 Unasema, "Ndugu Branham, je, hilo lilifanya lolote?"

109 Naam, bwana. Yesu alisema, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa Milele, wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Yesu alisema hivyo, Yohana Mtakatifu 5:24.

110 Sasa, ulipoinua mkono wako, wasema, "Hilo lililifanyia nini?"

111 Mbona, kulingana na kanuni za kisayansi, nguvu za uvutano huishikilia mikono yako chini, huwezi kuinua mkono wako. Lakini kulikuwa na Roho ndani yako, Uzima, aliyekuwa na mamlaka juu yako, Roho aliye karibu nawe ambaye alishuhudia kwamba umekosea, nawe ulitaka kuwa sahihi. Uliinua mkono wako kuelekea Muumba wako.

112 Sayansi inasema, kulingana na . . . Kama hakukuwa na roho ndani yako, mkono wako ungelazimika kuning'inia chini. Bali kuna roho ndani yako aliyefanya uamuzi na kuinua mkono wako. Mungu aliona hilo. Kama kweli ulimaanisha hilo, jina lako liliandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo. Hiyo ni kweli kabisa, ndugu, kama kweli unaamini.

113 Sasa, "Wote walioamini waliongezwa kwa Kanisa." Sasa, baada ya, kwamba tuuombee mstari huu wa maombi, ninawatakeni mje hapa juu. Simameni hapa, na hebu . . . hebu . . . tushuhudie hadharani. Kama utamkiri Yeye, ama kumshuhudia mbele za watu, "Nitakushuhudia mbele za Baba Yangu. Lakini kama unanionea aibu mbele za watu, nitakuonea

aibu mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu." Hivyo ndivyo Yesu alivyosema. Kwa hiyo njoni usiku wa leo, mara baada ya jambo hili.

114 Sasa, ni wangapi hapa ndani ambao wamemwacha Mungu, ambao hawamjui Mungu, na umeghairi ahadi yako kwa Mungu? Sasa, ninaamini ya kwamba kuhusu neema, ungali chini ya neema. Lakini ungetaka kumrudia Mungu, na useme, "Kama Roho Mtakatifu atakuja mkutanoni usiku wa leo na kufanya tu kama ulivyosema kwamba Yeye alifanya huko nyuma, hata wakamtambua, ninataka kumrudia Mungu na kumwomba ayajaze maisha yangu upya, na kunituma huko nje kwa ajili ya ushuhuda Wake kungali mchana."

115 Hutakuwa na wakati mwingine baada ya maisha haya kwisha kuwahi kumshuhudia Kristo, huna budi kufanya hivyo sasa. Waweza kuinua mkono wako? Useme, "Niombee." Nisipouona mkono wako...Mungu akubariki, bwana. Nisipouona mkono wako, hakika Mungu anauona. Vema. Mungu awabariki. Ninaomba ya kwamba Mungu atamjalia kila mmoja wenu.

116 Kadi hiyo ya maombi ilikuwa gani? F, kadi ya maombi F. Ni wangapi? Hamsini. Mwanangu alisema ya kwamba wao... Ninaamini yeye na Gene walisambaza kadi hamsini alasiri ya leo za F, kadi ya maombi F, moja hadi hamsini. Sasa, tutajaribu kuliombea kundi hilo lote usiku wa leo.

117 Sasa, hatutaki...Hutaki kuharakisha kama uwanja wa michezo, unataka tu kuwa na kicho kabisa, uketi kwa utulivu mpaka namba yako itakapoitwa.

118 Nani ana F? F, kama vile katika *father*. F namba moja, waweza kuinua mkono wako? Njoo moja kwa moja hapa, dada. Simama moja kwa moja nyuma hapa. Njoo moja kwa moja uzunguke pazia hapa. F, namba mbili, waweza kuinua ninii yako...? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...wanaamini. Sio kila mara tunapata imani kamilifu jukwaani, hatufanyi hivyo kila wakati.

119 Vema, ishirini na sita, ilikuwa hiyo? Ni nani aliye na ishirini na sita, kadi ya maombi ishirini na sita? Hiyo ilikuwa ni kweli? Ishirini na tatu. Ishirini na nne. Ni nani aliye na kadi ya maombi ishirini na nne, basi? Ilikuwa ni ipi, David? Ishirini na mbili. Ni nani aliye na kadi ya maombi ishirini na tatu, basi? Ishirini na tatu. Una ishirini na tatu ewe mama, unayekuja papa hapa? Ishirini na nne. Ni nani aliye na ishirini na tatu? Wewe mama? Ishirini na tatu. Vema. Ishirini na nne, ishirini na tano.

120 Kwa hiyo hatuninii, wote wasije wakasongamana na kuwatia watu wasiwasi, unataka kulijia jambo hili kwa uchaji, kwa utulivu, ukijua unachofanya. "Unakaribia kama kwenye Jiwe lililo hai, Kristo Yesu."

121 Ishirini na tatu, ishirini na nne, ishirini na tano, ishirini na tano, ishirini na sita, ishirini na sita, huko chini. Ishirini na saba, ishirini na saba. Vema. Ninaamini, labda wangeweza kuzunguka upande huu mwingine vile vile, labda. Ishirini na saba, ishirini na nane. Ni nani aliye na kadi ya maombi ishirini na nane? Ishirini na nane. Vema, vema. Njoni huko, basi. Ishirini na nane, ishirini na nane. Vema, ishirini na nane. Huyo mwanamke anaweza kutembea? Kama anaweza kutembea, sawa, hiyo ni sawa. Kama asingeweza, mbona, tutamleta mtu wa kusaidia kumwinua.

122 Ishirini na nane, ishirini na tisa. Kadi ya maombi ishirini na tisa. Vema, msichana. Thelathini, thelathini, thelathini na moja. Ni nani aliye na thelathini na moja?

123 Nimewashuhudia kitu ambacho ni kikubwa kuliko vyote ambacho kingeweza kushuhudiwa: kwamba Kristo yu hai. Wazia jambo hilo. Inamaanisha nini kwa nafsi yako?

124 Je, mnajua kuna dini nyingi mbalimbali, mamia ya hizo ulimwenguni ambazo zingekana jambo hilo, Wabudha, Waislamu, na kadhalika? Nadhani Ndugu Roberts, na labda Ndugu Tommy Osborn, pia, yupo, ambao ni wamishenari kutoka nchi za kigeni, wanaweza kuwaambia sasa hivi kwamba watasimama moja kwa moja na kuwaambia kwamba dini yao ina saikolojia kadiri yetu ilivyo nayo. Nao. . .Afadhali ujue unachozungumzia unapozungumza nao, hawaogopi.

125 Na sasa, lakini dini yetu ndiyo dini pekee iliyopo, dini ya Kikristo, inayoweza kuthibitisha ya kwamba Mwanzilishi wao yu hai baada ya miaka elfu mbili, mnaona, kwa sababu Uhai Wake unaishi katika Kanisa Lake. Hivyo ndivyo alivyoahidi.

126 Sasa, halafu ninaposimama hapa na hili. . .nikitoa madai haya ninayotoa, mnatambua hilo linamaanisha nini? Kuna angalau watu elfu moja hapa usiku wa leo, ningesema kwa urahisi watu elfu moja, nami nimekuwa na hao ambapo kungekuwa na watu elfu arobaini, ama, naam, mia moja na hamsini elfu, mia mbili elfu kwa wakati mmoja, wote wamechanganyikana kabisa na kwa kila njia, Yeye hajashindwa bado, wala hatashindwa, kwa sababu Yeye ni Mungu wala hawezi kushindwa. Kwa hiyo huna budi kuwa na hakika ya kwamba unajua kile unachozungumzia.

127 Sasa, sasa, vipi. . .? Ninyi watu huko nje msio na kadi za maombi na mnataka kuombewa. . .Sasa, mstari huu hapa si mstari wa upambanuzi, kamwe ni—nisingeweza kufanya hivyo, ingeniua. Ni wangapi wanaojua ya kwamba wakati Danieli alipoona ono moja, alifadhaika kichwani mwake kwa siku nyingi? Inua mkono wako. Vema.

128 Ni wangapi wanaojua ya kwamba mwanamke aligusa upindo wa vazi la Yesu, naye akamgusa, Naye akageuka, akasema, "Ni nani aliyenigusa?" Basi kila mtu akakana.

Aliangalia kwenye kusanyiko mpaka akampata huyo mwanamke, ndipo akasema, “Imani yako imekuokoa,” akamwambia kuhusu kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma kwa sababu imani yake, alimgusa.

129 Sasa, Yeye hakuhisi huo mguso wa kimwili, kwa sababu kulikuwa na watu wengi sana waliokuwa wakimgusa. Petro akamkemea, kasema, “Vema, kila mtu anakugusa, kwa nini unasema jambo kama hilo? Kila mtu anakugusa, usiseme hivyo.” Naye akamkemea.

Lakini Yeye akasema, “Naona kwamba nimeninii,” (Kitu gani?) “nguvu zimenitoka.” Ni wangapi wanaojua ya kwamba nguvu ni uweza? Hakika, alidhoofika.

130 Sasa, kama mwanamke mmoja kumgusa Mwana wa Mungu kulimfanya dhaifu, ningewezaje kuvumilia hilo, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema? Kwa sababu Yeye alisema, “Mambo haya nifanyayo, ninyi nanyi mtayafanya; na makubwa kuliko haya mtafanya.” Najua toleo la King James linasema *makubwa zaidi*, bali tafsiri yake halisi, kama mkiichunguza, ni “*mengi* kuliko haya mtafanya.” Mnaona? Kwa sababu Kanisa litakuwa la ulimwenguni kote na kustahimili mengi zaidi.

131 Sasa, lakini usingeweza kufanya makubwa zaidi, Yeye aliwaponya wagonjwa, akawafufua wafu, akasimamisha maumbile, akafanya kila kitu ambacho kingeweza kufanywa, usingeweza kufanya zaidi katika ubora, lakini zaidi katika wingi, kwa sababu Roho Wake angekuja na kuwa pamoja na Kanisa. Moja kwa moja usiku wa leo, wakati jambo hili likiendelea hapa, katika Afrika linaweza kuwa likiendelea, katika Australia linaweza kuwa likiendelea, kila mahali.

132 Lakini wakati Mungu alipokuwa hapa duniani katika umbo la mwanadamu, Yesu Kristo alikuwa ni Mungu aliyefanyika mwili na kuishi miongoni mwetu. Sasa, utimilifu wote wa Uungu kwa jinsi ya mwili ulikuwa ndani Yake, Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa. “Hakuna mtu aliyemwona Baba wakati wowote, ila Mwana wa pekee atokaye kwa Baba amemdhihirisha.” Ninii . . . Mungu alikuwa akijidhihirisha Mwenyewe, kile alichokuwa kupitia Mwanawe, Yesu.

133 Mungu alimtia uvuli bikira Mariamu, akaumba Seli ya Damu katika tumbo la uzazi. Na mtu yeyote anajua ya kwamba uhai hutokana na jinsia ya kiume. Hiyo ni kweli? Kuku anaweza kutaga yai, lakini kama hajakuwa pamoja na ndege wa kiume, halitaanguliwa, la, bwana, kwa sababu halina uhai ndani yake. Uhai hutoka kwa mwanamume.

134 Halafu basi katika kisa hiki Mungu alikuwa ndiye Mwanamume, wala hakukuwako na uhusiano wa kimwili naye hata kidogo, Mungu Muumba aliumba Seli ya Damu. Yeye hakuwa Myahudi wala Mmataifa, Yeye alikuwa ni Mungu. Hiyo ni kweli. Damu ya Yehova Mungu alijiumbia Mwenyewe Damu

ya kuwatakasa watu Wake. Ndipo basi ndani ya hiyo mlikaa utimilifu wa Mungu kwa jinsi ya mwili. Yeye alikuwa na Roho bila kipimo, tunaye kwa kipimo.

135 Sasa, kama ningeenda baharini na kuchukua, kama karama hii ndogo ambayo Yeye hunipa, kama ningeenda baharini na kuchota kijiko kimoja kutoka baharini, hiyo ni karibu kwa kulinganisha, karama hii ndogo hapa ni kama tu kijiko cha maji kutoka baharini, na Yake ilikuwa bahari yote. Lakini hivi ulijua, kama ukichunguza sehemu hiyo ndogo uliyo nayo ndani yako, na sehemu hiyo ndogo niliyo nayo ndani yangu, kemikali zile zile zilizomo kwenye kijiko hicho ziko katika bahari yote. Hakika. Ni kitu kile kile, sio kiasi hicho.

136 Tunaye Roho kwa kipimo, Mungu alitumwagia kwa kipimo, bali Yeye alimmiminia bila kipimo. Kwa hiyo kazi alizofanya Yeye, Kanisa Lake, alijitenganisha, akajigawa Mwenyewe miongoni mwa watu Wake, ili kazi Yake iweze kuendelea kupitia Kanisa Lake. Kama huo si upendo!

137 Si ajabu watu wanaingia wazimu. Na wimbo huu maarufu wa—wa "Loo, upendo wa Mungu, jinsi ulivyo mwingi na safi!" wananiambia ya kwamba aya hiyo, aya ya mwisho, ama aya ya kwanza, hasa, ninaamini, ama ya mwisho, ilipatikana imeandikwa kwenye ukuta wa hospitali ya wendawazimu. Hakuna mtu angaliweza kuuwazia kwa kalamu, ama hakuna njia ya kujaribu kuonyesha upendo wa Mungu.

> *. . .Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, . . .kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa* Milele.

138 Ni mwaliko wa jinsi gani ambao Yehova Mungu aliwapa watu Wake!

139 Marafiki, tunapaswa kuona aibu kwa kutomtumikia. Sasa, mnafahamu ya kwamba haya nilisema ni kijiko kimoja. Sasa, Yeye yupo hapa sasa katika mkutano huu, Kristo yupo hapa. Mnaamini hilo?

140 Sasa, mpate kujua: Kuna mtu yeyote mkutanoni hapa ambaye hajawahi kuwa katika mmoja wa mikutano yangu hapo kabla? Inueni mikono yenu, ambao hawajawahi kuwemo. Loo, jamani! Nusu ya umati, zaidi ya nusu. Unapata wapi kila wakati?

141 Sasa, si—siwezi kuchukua wakati. Hii. . .Hapa, ninyi nyote huko nje mnaomwamini Mungu, msio na kadi ya maombi, hebu upambanuzi uwe huko nje. Mnaamini mna imani ya kutosha kugusa vazi Lake? Mnaamini hilo? Mnaamini mna imani? Kama mnaamini, vema, mnaweza kuupokea.

142 Sasa, kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, mnaamini hilo? Mnaamini hilo kwa dhati? Vema, hivi Yeye ni Kuhani Mkuu anayeketi mkono wa kuume wa Mungu sasa, na anaweza kutuombea tunapokiri, na Yeye ni Kuhani Mkuu

anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Mnaamini hilo? Ninyi wageni mnaamini hilo? Vema, basi huyo Kuhani Mkuu angetendaje kama ungemgusa usiku wa leo? Kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, angetenda vile vile kama alivyotenda wakati huo. Basi mwanamke yule alipogusa vazi Lake, aliona kwamba yeye alikuwa ni nani, akamwita, na kumwambia, kuhusu kile alichokuwa nacho (Hiyo ni kweli?), na kutamka ya kwamba imani yake ilikuwa imemponya.

143 Sasa, mnaamini jambo lile lile? *Ninyi* ombeni. *Ninyi* ombeni. Hii hapa changamoto: Hebu upambanuzi uwe huko nje. Hawa ni watu tu wanaosimama kwenye mstari wa maombi.

144 Sasa, kama ninyi watu mnaosimama hapa kwenye mstari wa maombi mnaweza kuangalia huko nje, hamtaninii... Mnatambua ya kwamba...Ninaninii tu, ninaweza tu kuomba na kuwawekea mikono. Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.” Si mikono yangu tu, bali kila mkono hapa ndani, kwa imani, utawekwa juu yenu kwa ajili ya uponyaji wenu.

145 Hatuko hapa kuonyesha, tuna...sisi si watu wa maonyesho. Sisi ni Wakristo, tuko hapa ku—kudhihirisha na kuwapa Injili ya Mungu. Mungu alifanya ahadi, akatuma karama.

146 Wahudumu hapa ndani, karama Kanisani ni nini? “Mungu ameweka Kanisani, kwanza mitume.” Hiyo ni kweli? Ama *wamishenari*, ni jambo lile lile, yote mawili yanamaanisha, “aliyetumwa, mtu aliyetumwa.” Mitume, manabii, waalimu, wainjilisti, na wachungaji, Mungu aliwaweka kwa neema Yake Mwenyewe na kujua Kwake tangu zamani Kanisani.

147 Sasa, katika kila kanisa la mahali hapo kuna karama tisa, kama vile kunena kwa lugha, na kufasiri lugha, na hizi zingine zote, ambazo mmefundishwa kuzihusu. Sasa, hilo linadhihirisha tu, itakuwa juu ya mmoja usiku wa leo, na mwingine usiku mwingine. Lakini sasa, kama Kristo anaishi miongoni mwetu, na atuthibitishie, usiku wa leo, ya kwamba Yeye yuko.

148 Sasa, ninyi mlio na imani na mnaamini. Na jalia iwe angalau mbili ama tatu kuthibitisha ya kwamba nimesema kweli. Popote katika kusanyiko hili, anzeni kuomba na kusema, “Mungu, jalia huyu mtu anene nami, nami nitajua Huyo siye.” Hakuna mtu ninayeweza kumwona...Nyote katika mstari huu wa maombi, tusiofahamiana, inueni mikono yenu, kila mmoja wenu ambaye hatufahamiani. Kote katika kusanyiko hapa ambao hatufahamiani, inueni mikono yenu, wote ambao hatufahamiani.

149 Sasa wewe omba, uone kama Kuhani Mkuu angali anaishi kufanya maombezi, uone kama ungali unaweza kumgusa, fanya hivyo. Ndipo itakuondolea mashaka yote. Ombeni tu.

150 Tunazo picha Zake hapa, zimepigwa kote ulimwenguni huko Ujerumani, na Marekani, na Canada, na kila mahali. Kisayansi,

imetundikwa kwenye ukumbi wa sanaa za kidini huko juu, imethibitishwa kisayansi. George J. Lacy mkuu wa FBI wa alama za vidole na hati alisema, alitia sahihi hati hiyo mwenyewe, "Nuru iligusa lenzi." Akasema, "Nilikuwa siamini hilo, pia, lakini kamera haitapiga picha saikolojia." Si saikolojia.

151 Hapa, mama huyu aliyeketi hapa ameinamisha kichwa chake, akiomba, aliyeketi moja kwa moja mbele yangu, unataka kuondokana na hizo bawasiri, sivyo? Naam. Nawe una upepo mdogo kichwani mwako, sivyo? Vema, imekwisha sasa. Nenda nyumbani ukapate afya.

Unaamini?

152 Mwanamke huyu aliyeketi papa hapa mwishoni huku ameinua mkono wake kinywani mwake namna *hii*, unataka kupona hicho kisukari na upate afya? Unaamini ya kwamba Yesu Kristo atakuponya? Vema, basi nenda nyumbani ukaponywe, Yesu Kristo atakuponya.

153 Mtu huyu aliyeketi hapa mwenye shinikizo la juu la damu, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, bwana, uliyeketi hapo nyuma? Unaamini? Vema, simama kwa miguu yako. Mimi . . . Mtu huyu papa hapa aliyevaa tai nyekundu hapo, sikujui, wewe ni mgeni kwangu, lakini nenda nyumbani na uwe mzima, Kristo anakuponya.

154 Sasa, mnaamini, ninyi watu hapa kwamba, kwa mara yenu ya kwanza?

155 Hapa, ni yupi—ni yupi wa kwanza? Huyu—huyu—huyu—huyu . . . ? Wewe ndiwe yule mama? Njoo hapa kwa dakika moja. Simama papo hapo kwa dakika moja tu.

156 Mimi na wewe hatufahamiani? Mungu anatujua sote wawili, nasi hatufahamiani. Sasa, huyu hapa mwanamke, huu *hapa* mkono wangu, sijawahi kumwona maishani mwangu, nijuavyo mimi. Kusudi upate kuona ya kwamba thibitisho lisiloweza kukosea kwamba Kristo, Roho Mtakatifu, yupo hapa. Unaona?

157 Sasa, sasa kama—kama Roho Mtakatifu atanifunulia . . . Kama ningesema, "Mama, wewe ni mgonjwa." Vema, hiyo yote ni kweli, wewe—wewe labda ni mgonjwa. Lakini kama Yeye angeniambia . . . Niseme, njoo, nikuwekee mikono yangu, nami niseme, "Mungu atakuponya, ninaweka mikono yangu juu yako." Una haki ya kuamini hilo. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Ningesema, "Roho Mtakatifu yupo hapa." Hiyo ni kweli, ninaamini hilo. Lakini sasa, kama Yeye angekwambia jambo fulani ambalo umefanya ama jambo fulani kama nililozungumzia kuhusu Yeye kufanya, usiku wa leo, katika Maandiko, basi ungejua ingebidi iwe ni nguvu fulani, maana sikujui, sijawahi kukuona.

158 Hiyo ingekuwa ni kweli, enyi wasikilizaji? Kwenu ninyi watu ambao hamjawahi kuwa mkutanoni hapo awali, inua

mkono wako kama hiyo—hiyo ingekuwa ni kweli, mnafikiri hilo lingekuwa sahihi. Sasa, huu *hapa* mkono wangu, huyu mama hanijui, simjui, tunasimama tu hapa. Hii ni picha tu ya Yohana Mtakatifu 4, mtakapoenda nyumbani . . . Yesu na . . . alikutana na yule mwanamke kisimani, mwanamke Msamaria, na kumwambia shida yake. Kuna mtu anayekumbuka hilo? Tulikuwa nalo katika ujumbe usiku wa leo. Hili hapa tena, papa hapa usiku wa leo, papa hapa vile vile.

159 Roho Mtakatifu . . . Huyu mwanamke, simjui. Huenda asiwe Mkristo, huenda akawa mgonjwa, huenda akawa katika matatizo ya kifedha. Simjui, sijawahi kumwona maishani mwangu, lakini kama Kitu fulani kikizungumza naye, basi utajua ni Nguvu fulani. Sasa, ni juu yako kuamini kile Kilicho, ni juu yako. Kumbuka, kama ukikishuku, basi nyamaza nacho, kwa sababu, "Neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe," alisema Yesu, "katika ulimwengu huu, wala ulimwengu ujao."

160 Sijui kwamba Yeye angelisema. Lakini Bwana akipenda, ataninii . . . utajua kama hiyo ni kweli ama si kweli, utajua. Sasa, wewe ni Mkristo, nami sisemi hivyo kwa sababu umesimama hapo ukisema jambo fulani kwa midomo yako, ukiomba, silisemi hivyo, kwa sababu kama . . . ungeweza kuwa unasema hivyo, na bado uwe unajifanya tu. Lakini wewe ni Mkristo, hiyo ni kweli, kwa sababu ninajua ya kwamba roho yako inajisikia kukaribishwa. Nawe unajua ya kwamba jambo fulani linaendelea sasa hivi, hisi tamu sana, nyenyekevu. Kati yangu na wewe inasimama ile Nuru, ikitembea.

161 Sasa, unataka nikuombee kwa ajili ya kivimbe, na kivimbe hicho kiko chini ya mkono wako wa kulia, ni kitu kama kifundo. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Bi. Lindsey, unaweza kwenda nyumbani ukaponywe. Yesu Kristo . . .? . . .

162 Unaamini sasa kwa moyo wako wote? Sasa, hebu sote tuendelee kuomba, tuwe katika hali ya maombi.

Njoo, dada.

163 Sasa, Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utampa afya, katika Jina la Yesu.

164 Sasa, unajua ya kwamba ningejua shida yako mbali na tezi yako, na kadhalika. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya?

165 Mungu Mbinguni, uturehemu na uponye . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

166 Je, ungetaka nikwambie shida yako? Unataka nikwambie? Ni shida ya wanawake, shida ya kike. Hiyo ni kweli, sivyo? Sasa, nenda zako tu ukiamini. Unaona, kuwa tu na imani.

Sasa njoo, bwana.

167 Ee Bwana, ninaomba ya kwamba utamsaidia ndugu yetu mpendwa na kumpa afya, ninapomwekea mikono, katika Jina la Yesu.

Njoo ndugu yangu.

168 Baba Mungu, mponye ndugu yetu, ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

169 Njoo, dada. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya sasa tunapoomba? Sasa, usiwe na shaka.

170 Sasa, Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya na kumpa afya, katika Jina la Yesu.

Njoo, dada. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

171 . . .kuwaambia kuna shida gani, ono halikuponyi, imani yako katika Mungu ndiyo inayokuponya. Mnaona, Yeye angali hapa, hakumgusa tu huyo na—na kuondoka.

172 Hapa, njoo hapa, bwana. Unaamini kama Mungu anaweza kuniambia shida yako ni ipi, kwamba—kwamba u—uliamini ingekuwa ni Mungu, sivyo bwana? Vema. Bila shaka, sasa kile unachotaka nikuombee ni hicho kivimbe usoni mwako. Hilo ndilo unalotaka. Sasa, ngoja kidogo tu tuone kama Roho Mtakatifu angesema jambo lingine. Unaona?

173 Sasa ninii tu, bila shaka, mnaona hiki kivimbe usoni mwake. Mara tu aliposimama hapa, niliona hicho ndicho alichotaka, mnaona, kivimbe usoni mwake. Vema, bwana. Naam, bwana. Hicho ndicho unachotaka kiombewe, ni kivimbe usoni mwako.

174 Unaonekana kuwa mtu mzuri, naam, mhudumu. Hiyo ni kweli. Wala wewe pia hutoki hapa, unatoka nchi nyingine, ni nchi yenye misitu, kila mahali, unatoka Arkansas. Nawe, unamwombea mtu fulani huko Arkansas, mtu huyo ana kansa. Wakati mmoja uliponywa kansa, nayo hiyo kansa ilikuwa shingoni mwako, ikaombewa, ikaanguka. Hiyo ni kweli. Hiyo ilikuwa huko Jonesboro. Hiyo ni kweli. Hiyo ni, BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli.

175 Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Kasisi Bw. Shepherd, hicho kitaondoka usoni mwako kama utaliamini. Nenda, na umwamini Mungu, na uamini kwa moyo wako wote. Mungu akubariki. Liamini, ni hayo tu . . .? . . .

176 Kila mtu awe tu katika maombi sasa, kila mtu akiwaombea watu hawa wagonjwa. Vipi kama ni mama yako, na kadhalika, anayekuja?

177 Ninaomba ya kwamba utayafungua macho ya ndugu yetu na kumjalia apone, katika Jina la Yesu. Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

178 . . .Mungu, naweka mikono juu ya huyu mwanamke, jalia aponywe katika ninii la Yesu . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

179 Yule mvulana mwenye macho yaliyopofuka, yalifunguka alipokuwa akishuka kwenye hivi vipandio. Hebu tumpe Mungu sifa, kila mtu.

[Ndugu Branham anaendelea kuwaombea wale walio kwenye mstari wa maombi, mengi ya maneno yake hayatambuliki—Mh.]

Mlete huyo mvulana mdogo . . . ? . . .

"Kama tu unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana."

Unaamini kama ningeuliza . . . ? . . .

Bwana, katika Jina la Yesu . . . ? . . .

Mungu akubariki, rafiki. Amini sasa.

Njoo, mama. Mungu ni Mungu mkuu.

Baba, katika Jina la Yesu . . . ? . . .

Njoo ukiamini. U hali gani, dada? Unaamini atapona kama nitaomba?

Baba wa Mbinguni mwenye fadhili, ninaomba katika Jina la Yesu, kama unaweza kuyarejesha macho ya vipofu . . . ? . . . turehemu, Baba, ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Usitie shaka . . . ? . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

. . . ninyi nyote mnaamini kwa moyo wenu wote? Mnaamini? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

180 Je, aliombewa? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Hiyo ingeweza kuwa . . . Angalia, unaona, unaamini Mungu anaweza kuniambia jambo lingine kukuhusu? Unaamini? Hilo lingekufanya uamini zaidi? Kwa sababu hilo ni jambo zito, huna budi kuwa na nyongeza kidogo tu ya imani. Unaamini ya kwamba Yeye anaweza kuniambia? Kivimbe hicho ndicho unachotaka kiombewe, bila shaka, una udhaifu, na halafu una wasiwasi kuhusu jambo fulani. Ni kuhusu, naam, kwamba una mpendwa unayetaka aombewe, huyo alikuwa ni mume wako. Alikuwa hapa mkutanoni, na ilimbidi kuondoka kwenda nyumbani. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Bibi Austin. Nawe unaweza kwenda nyumbani na uwe mzima. Amini kwa moyo wako wote . . . ? . . .

181 Usiwe na shaka. Amini. Aminini. Kila mtu, amini sasa kwa moyo wako wote. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

182 . . . ombeni ya kwamba atapokea uponyaji wake, pia, anapopitia kwenye mstari huu. Laana na imwache, katika Jina la Yesu. Amina.

183 Vema. Sasa aminini. Hiyo ni kweli, ndugu. Nenda, ukiamini . . . ? . . . ukiamini.

184 Njoo, dada. Amini tu kwa moyo wako wote unapoenda.

185 Sasa, Baba yetu wa Mbinguni mwenye fadhili, ninaomba ya kwamba utambariki dada yetu na kumponya katika Jina la Yesu. Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

186 . . . unapopitia mstarini, kama tu uko chini ya msalaba, amini ya kwamba unapitia chini ya maombi ya watu hawa.

187 Baba, katika Jina la Kristo jalia dada yetu aponywe. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

188 . . . au utakufa kwa kansa hiyo, bali unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Sasa, ni jambo la kuogofya, bali lile giza limekuacha. Hilo limekuacha sasa, kama utaamini, kansa hiyo haitakuua kamwe. Nenda zako . . . ? . . .

Njoo, dada. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

. . . kwa ajili ya rehema kwa ajili yake. Amina.

Ninaamini ile . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

189 Hivi wewe . . . ? Je, hii . . . ? . . . Samahani, bwana, nilifikiri walikuwa kila mahali. Nilikuwa nikishuka kuja kwa huyo mama. Wakati mwingine maono hayo hunifanya dhaifu nayo . . . Vema, ninyi . . . Kujiondoa tu kwenye kusanyiko, na kadhalika, sana—sana. Unaamini? Hilo ni zuri sana. Hilo ni zuri sana. Hilo ni . . . Ugonjwa wako wa kisukari umekusumbua sana. Unaamini ya kwamba Kristo atakuponya hicho kisukari?

190 Una tabia ambayo huna budi kuiacha, pia, kuvuta sigara. Hiyo ni kweli. Na jambo lingine, unamhitaji Yesu kama Mwokozi wako, giza limekuzunguka, wewe si Mkristo. Je, utamkubali sasa kama Mwokozi wako binafsi? Unamkubali kama Mwokozi wako? Vema. Bw. Perry, hilo ndilo jina lako, Bw. Perry, umeokoka sasa, Kristo anakusamehe dhambi zako, anakuponya ugonjwa wako. Nenda zako ukapate afya, katika Jina la Yesu Kristo.

191 Unaamini kwa moyo wako wote? Kila mtu anaamini? Sasa, sijui kama hao watu walioinua mikono yao dakika chache zilizopita: Je, unaamini ya kwamba Mungu husikia maombi? Waweza kuja hapa na kusimama papa hapa kwa dakika moja tu? Je, ungetaka kushuka moja kwa moja hapa wakati ukiwa Mbele za Roho Mtakatifu, kwamba ungetaka kuja moja kwa moja hapa chini tunapoimba wimbo? Ninyi nyote mnaomhitaji Kristo, mwaweza kuja papa hapa dakika moja tu, ambaye unataka kumkubali kama Mwokozi wako binafsi? Njoni hapa. Mbele Zake, kamwe hamtawahi kuwa karibu zaidi.

192 Nawaambia, marafiki, natumaini hamnihesabu kuwa mlokole, ninawaambia kweli, Roho wa Mungu yuko mkutanoni sasa. Mnajua hilo bila shaka lolote.

193 Sasa, tunapoimba wimbo. Tutaimba nini? Ati nini? *Nampenda*. Tunapoimba, *Nampenda*, kutoka kwenye roshani, tutawangojea, shukeni mje hapa na msimame hapa kwa ajili ya maombi mafupi tu ya kibinafsi, mkiweza, papa hapa chini.

Njoni, hebu watu wajue ya kwamba kweli unamwamini na unataka kumkubali. Moja kwa moja Mbele Zake sasa, shukeni moja kwa moja na kusimama hapa kwenye hili—hili shimo pamoja nami kwa dakika chache tu. Mtafanya hivyo sasa? Tunapoimba, *Nampenda*. Vema, Ndugu Borders.

Nampenda, nampenda

Utakuja moja kwa moja sasa, wewe uliyeinua mkono wako?

Kwani Yeye . . .

Njoo moja kwa moja kutoka kwenye roshani. Hiyo ni kweli.

. . . alinipenda
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

194 Marafiki, ninataka kuwaulizeni: Umewahi kuwazia utakuwa karibu zaidi ya ulivyo sasa hivi, mpaka utakapoona umbo Lake linaloonekana? Yuko hapa. Mimi ni ndugu yenu, mimi ni mwanadamu tu kama mlivyo ninyi. Lakini nikiweza tu kujisalimisha kwa Roho na kustarehe, Yeye hufanya mambo hayo. Sasa, mimi ni dhaifu sana, kwa kuwa unaweza kuona jasho likitiririka kutoka mkononi mwangu . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] " . . . wokovu Kalvari." Hivi hutakuja sasa?

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Kalvari . . .

195 Bwana anayezijua siri za moyo wako anaweza kuwamfanya vipofu kuona, viziwi kusikia, bubu kunena, Uwepo Wake wenye upendo upo hapa. Hivi hutatoka sasa? Kama umerudi nyuma, mbali sana na Mungu, baridi moyoni mwako, unataka tukio jipya pamoja na Mungu, si ujitokeze? Au hata kama hujampokea Roho Wake Mtakatifu, kwa nini usisogee juu sasa hivi? Njoo hapa na . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

196 . . . hawayajui Maandiko. Usitumie miujiza ya Ufunuo 11 katika wakati wa Mataifa, hiyo ni kwa ajili ya Wayahudi. Basi moja ya siku hizi Mungu ataniruhusu niende Yerusalemu. Ndivyo itakavyokuwa. Kumbukeni tu, kama mnaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu, Wayahudi watakapompokea Kristo kama Masihi, Mataifa wamekwisha. Ni saa yako, afadhali uje. Mara nyingine tena, ili nipate kuwa na hakika ya kwamba haitanibidi kujibu kwenye Siku hiyo, mara nyingine tena:

Nampenda . . .

Ndugu wahudumu, tokeni mje hapa, hivi mtakuja?

. . . mpenda
Kwani (Hiyo ni kweli.) alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

197 [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nampenda*—Mh.] Loo, Uwepo wa Utu Wake! Shuka uje moja kwa moja. Jambo ndilo hilo, dada. Njoo moja kwa moja, ndugu mpendwa.

Mtini Kalvari.

198 Baba wa Mbinguni, sasa tunakuletea, katika Jina la Mwanao, Bwana Yesu, hawa waliotubu wanaosimama wakikabili kusanyiko. Wanajutia dhambi zao, wao ni nyara za mkutano huu, nyara za neema Yako na Uwepo Wako. Imeandikwa katika Maandiko ya kwamba "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza." Halafu basi pia imeandikwa, "Wote alionipa Baba, watakuja Kwangu."

199 Ni watu waliojaliwa jinsi gani usiku wa leo kujua ya kwamba Mungu Mwenyezi amewavuta kwa Mwanawe, Yesu! Ni zawadi za upendo ambazo Mungu anampa Mwanawe, Kristo Yesu. "Hakuna mtu awezaye kuwatoa mkononi Mwangu," alisema Yesu. Wako hapo, wamelindwa salama.

200 Wanakuja juu ya imani ya roho yao, Bwana, Roho Mtakatifu akiwaleta Mbele Zako. Wameshawishika ya kwamba wa—wamekosea, nao wanataka Uzima wa Milele. Ulisema, "Wote waaminio, wanaupokea Uzima huu wa Milele." Nawe ulisema ya kwamba ungewafufua katika siku ya mwisho.

201 Na kuwazia kwamba wakati jua lenye joto limeanza kuilowesha dunia, maskini maisha yaliyojificha ya maua hayo yaliyoko mavumbini, ambapo hakuna mwanasayansi angaliweza kupata chembe hiyo ya uhai, bali yalikaa mavumbini, nayo mazingira mazuri tu ya jua hilo yaliyachipusha hayo maua madogo, yanakuja kila mahali. Hapo ndipo jua, lile j-u-a linalofufua uhai wa mimea lilichipusha hilo ua.

202 Siku moja Mwana wa Mungu atakuja. Nao watu hawa, usiku wa leo, wanaosimama hapa kuupokea Uzima wa Milele, mbele ya kusanyiko hili, mbele ya watumishi Wako, wahudumu hawa, sasa wanasimama hapa kuukubali Uzima wa Milele, na siku moja huenda ikawa, wataingia mavumbini, huenda kukawa na jeneza watakalolalia, matope yamwagwe mwilini mwao, jiwe la kaburi lijengwe, bali hawawezi kuuficha Uzima wa Milele. Yesu atakapokuja, watatokea, kwa sababu Wewe uliahidi jambo hilo.

203 Tunawakabidhi Kwako, Bwana, nao ni nyara. Jalia waishi maisha marefu hapa duniani yaliyojaa furaha na amani. Jalia wapate nyumba nzuri, kanisa zuri la nyumbani, na hapo wabaki waaminifu kwenye wajibu wao, mpaka mauti yatakapowaweka huru kutoka kwenye safari hii ya duniani. Tujalie, Baba. Wao ni Wako, katika Jina la Kristo.

204 Ninyi mnaosimama karibu na madhabahu, ninyi mliokuja kutubu, sasa unamwamini na kumkubali Yesu kama Mwokozi wako binafsi, ukiamini ya kwamba wewe, kwamba yote unayoweza kufanya ni kuzisikitikia dhambi zako? "Yeye

aombaye hupokea." Kama unaamini, waweza kuinua mikono yako kwamba sasa utaziacha dhambi zako na kumkubali Yesu kama Mwokozi wako? Inueni mikono yenu, kote kwenye madhabahu. Ajabu! Bwana Mungu awabariki.

205 Sasa, ndugu, wahudumu, ninawatakeni mje karibu nao, mahali walipo, muwawekee mikono, kisha tutawaombea kwamba wapokee ubatizo wa Roho Mtakatifu papo hapo wanaposimama. Njoni moja kwa moja karibu nao, kila mmoja wenu, njoni huku karibu na kila mtu. Ninyi wahudumu hapa, kusanyikeni hapa, na kuwawekea mikono ya kwamba watapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.

206 Sasa, wasikilizaji wengine, inamisheni vichwa vyenu katika maombi wanapoomba, pia.

207 Ndugu du Plessis, njoo hapa uongoze maombi haya, tafadhali, tunapoomba…?…

60-0329 Ni Mimi, Msiogope
Municipal Auditorium
Tulsa, Oklahoma Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org